# Dhana ya Lafudhi katika Isimu: Mifano kutoka Lugha ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kibantu

Michael A. Mashauri


## Iksiri

Makala hii inalenga kuitalii dhana ya lafudhi kama inavyotumika katika isimu na kujaribu kuongeza kile ambacho hakijagusiwa na wanaisimu waliotangulia ambao walijishughulisha kwa namna moja ama nyingine kuiandikia dhana hii. Wataalamu wengi wemeizungumzia dhana ya lafudhi na kuitolea mifano ya tofauti za kivitamkwa pekee bila kuhusisha vipengele vingine ambavyo pia vinahusika katika kuitambulisha lafudhi ya mzungumzaji wa lugha fulani au wa mahali fulani. Makala hii inajaribu kuubainisha undani wa dhana ya lafudhi kuwa haihusishi vitamkwa tu bali pia vipengele vingine vya kimatamshi. Mifano iliyotumika inatoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu, Kibena, Kifipa, Kihaya na Kinyamwezi. Aidha, mifano mingine kutoka katika lugha ya Kiswahili inatokana na utamkaji wa maneno ya Kiswahili kwa kutumia lafudhi ya Kiarabu kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili walioathiriwa na utamkaji wa lugha ya Kiarabu.


## 1.0 Utangulizi

Makala hii inaielezea dhana ya lafudhi katika taaluma ya isimu kwa kutumia mifano mbalimbali kutoka katika lugha za Kibantu ambazo ni Kiswahili sanifu, Kibena, Kifipa, Kihaya na Kinyamwezi. Pia, lugha nyingine kama vile Kimasai, Kikurya, Kimakonde, na Kiluo zimegusiwa, hususani katika kuangalia mifano iliyotolewa na wataalamu wengine ambao tumewajadili katika makala hii. Katika kuitalii dhana hii tumeigawanya makala katika sehemu tano: sehemu ya kwanza ni utangulizi; sehemu ya pili ni ufafanuzi wa dhana ya lafudhi kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali; sehemu ya tatu inaonyesha na kuijadili mifano mbalimbali ya lafudhi inayotolewa na wataalamu na dosari za ufafanuzi wa dhana hii na mifano inayotolewa; mambo ambayo yanahitaji kujadiliwa na kufanyiwa kazi katika makala hii; sehemu ya nne inaeleza msimamo wa makala hii kuhusiana na dhana ya lafudhi. Sehemu hii ya nne imegawanyika katika sehemu ndogo tatu ambapo sehemu ya kwanza inafafanua dhana ya lafudhi kwa ujumla na vipengele vyake kama vile vitamkwa, toni, mkazo, kiimbo, wakaa na tambo. Sehemu hii inafuatiwa na maelezo kuhusu aina za lafudhi ambazo ni lafudhi-nafsia na lafudhi-jamii. Sehemu ya tano ni hitimisho.

## 2.0 Dhana ya Lafudhi

Dhana ya lafudhi imejadiliwa na wataalamu wengi ambao kimsingi wametoa fasili na mifano inayokaribiana sana. Katika makala hii tutawataja wachache na kuonyesha jinsi wanavyoifasili dhana hii na kuijadili mifano yao. Katika kitabu cha Massamba na wenzake (2004:10) lafudhi imefasiliwa kuwa ni sifa ya kimasikizi (inayohusiana na kusikika kwa sauti wakati wa kutamka) ya matamshi ya mtu binafsi ambayo humpa msemaji utambulisho fulani ama kijamii au kieneo

(kijiografia). Kwao, usemaji kuweza kumtambulisha mtu kimazingira ya kijamii na kijiografia ni kipengele muhimu katika kuitambua dhana ya lafudhi. Mazingira haya ya kijamii, kwa hakika, yanamaanisha athari za lugha ya kwanza katika usemaji wa lugha ya pili. Kwa kuwa lugha ni zao la jamii na kila jamii huwa na mazingira yake ya kijiografia au kieneo inamopatikana, ndiyo maana suala la mazingira ya kijiografia limehusishwa na lafudhi.

Aidha, Massamba (2004:44) anaigawa dhana ya lafudhi katika aina mbili ambazo ni *lafudhi* na *lafudhi kali*. Lafudhi ina maana ya utamkaji maneno wa mtu ulio wa kawaida. Katika usaili tuliofanya naye ofisini kwake tarehe 30/03/2015 Massamba alisema kuwa “aina hii ya lafudhi ni ule utamkaji unaomtambulisha mtu binafsi miongoni mwa wanajamii wenzake ambao unaweza kuwa katika lugha ileile.” Hii ina maana kwamba wakati mtu anapotamka maneno katika uzungumzaji wake kuna msikiko wa sauti yake wa kipekee na namna ya utamkaji aliyo nayo ambayo inamtambulisha yeye kwa jina lake katikati ya jamii fulani yenye lafudhi yake ya kijamii. Ili dhana hii iweze kueleweka vizuri zaidi tunaweza kuona mfano pale ambapo mtu mmoja anapokuwa ndani ya nyumba halafu akasikia mtu mwingine anaongea nje ya nyumba na yule wa ndani akamtambua kuwa huyo ni fulani na si fulani. Utambuzi huu huja kwa kutumia msikiko wa usemaji wake katika jamii ileile. Mfano mwingine ni ule tunaoweza kuuona kwa wale wenye ulemavu wa macho ambao husikia tu usemaji wa mtu na kumtambua kuwa huyu ni fulani ingawa wote wanazungumza lugha ileile.

Kwa upande wa lafudhi kali anasema kuwa ni matamshi ya msemaji ambayo yanaonyesha athari za ama anakotoka, mazingira alimo au lugha yake ya kwanza. Kwa hiyo, kwa mujibu wa fasili hii, utamkaji wa maneno unaomtambulisha mtu kuwa ni mzungumzaji wa lugha fulani kama lugha yake ya kwanza na kwamba anatoka eneo fulani inakosemwa lugha hiyo unaitwa lafudhi kali. Tutarejelea zaidi kuhusu dhana ya lafudhi na lafudhi kali katika sehemu ya tatu ya makala hii.

Kwa mujibu wa TUKI (2004:203) lafudhi ni matamshi ya mzungumzaji yanayotokana na lugha yake ya mwanzo au lugha zinazomzunguka. Aidha, wanaendelea kusema kuwa ni udhihirishaji wa sauti za lugha unaomtambulisha mtu mmoja au jamii ya watu. Fasili na maelezo haya yanaoana na yale ya wataalamu tuliowajadili hapo juu kuwa lafudhi inatokana na matamshi ambayo kwa asilimia kubwa hutokana na usemaji wa lugha ya kwanza ya mtu. Utamkaji huo unamtambulisha msemaji mmoja au jamii nzima ya wale wanaozungumza lugha hiyo iliyowaathiri. Kusema kuwa ni usemaji unaomtambulisha msemaji mmoja au jamii kunaonyesha kwamba wataalamu hawa wana wazo linalofanana na Massamba (2004) anaposema kuwa kuna lafudhi na lafudhi kali ila tu hawakuendelea zaidi kufafanua dhana hii. Inawezekana kabisa kuwa ule usemaji unaomtambulisha mtu mmoja ndiyo lafudhi kwa mujibu wa Massamba (2004) na ule unaoitambulisha jamii

kuwa kama lafudhi kali. Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa fasili zote hizi zinakaribiana sana.

## 3.0 Mifano ya Lafudhi Inayotolewa

Wataalamu walioizungumzia dhana ya lafudhi katika lugha za binadamu, hususani wale wanaoandikia isimu ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu, wametoa mifano ya lafudhi inayohusisha vitamkwa tu. Mathalani, Ali (1976) ambaye aliizungumzia lafudhi ya Kiswahili sanifu kwa kutoa mifano ya vitamkwa peke yake. Yeye anasema kuwa katika lafudhi kuna herufi ambazo zinawakilisha sauti mbalimbali. Katika kazi yake yote anaitazama lafudhi kama sauti tu (ambazo yeye anaziita herufi). Aidha, Maganga (1976) naye amelijadili suala la lafudhi kwa kutumia kiimbo peke yake akitoa mifano ifuatayo:

(a) Nimeisha mwona/yule jamaa/tayari;
(b) Nimeisha muona yule jamaa/tayari; na
(c) Nimeisha/muona/yule/jamaa/tayari.

Alama / katika mifano hii inaonyesha mipaka ya kiimbo (alichokiita *kikoromo*) ambayo lafudhi za watu huweza kutofautishwa kulingana na utumiaji wao wa kiimbo.

Wataalamu wengine ni Massamba na wenzake (2004:10) wanatoa mifano ya lafudhi kama ifuatavyo:

(a) Usirete matata mura (msemaji atakuwa ni Mkurya);

(b) Unapaswa kujua kuwa kwetu kuna mgomba siyo ngombe (msemaji atakuwa ni Mhaya);

(c) Baba kaleta nchicha na nkate ya ntoto (msemaji atakuwa ni Mmakonde);

(d) Amekuya kutumika fasi ya Katibu Mkuu (msemaji atakuwa anatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Mkongo);

(e) Wee mitu kabila gani hapana kojoa Kiswahili msuuri (msemaji atakuwa ni Mluo); na

(f) Hero rafiki nataka ile shuma nakula shuma ingine (tupa) (msemaji atakuwa ni Mmasai).

Ukitazama mifano hii utaona kwamba inazungumzia lafudhi kwa maana ya:

a) kubadilisha sauti moja au kitamkwa na kuingiza sauti inayotokana na lugha ya kwanza ya msemaji huyo; kama vile katika (a) kuna /r/ badala ya /l/, “usirete” badala ya “usilete”; katika (d) kuna “amekuya” badala ya “amekuja”.

b) Udondoshaji wa kitamkwa kama vile katika (e) inaposomeka “wee” badala ya “wewe” na katika (f) kuna matumizi ya “ingine” badala ya “kingine”, hivyo sauti /k/ imedondoshwa.

c) Kutofuata upangaji sahihi wa viambishi vya upatanifu wa kisarufi (ambao pia bado ni vitamkwa) kama vile katika (e) “mitu” badala ya “mtu”, “Kiswahili msuuri” badala ya “Kiswahili vizuri”.

d) Kushindwa kutamka maneno vizuri kulingana na jinsi yanavyotamkwa katika lugha ya Kiswahili, kama vile katika (e) “kojoa” badala ya “kujua”. Hapa mtamkaji ameshindwa kutamka sauti /u/ na kutamka /ɔ/ mahali pa /u/. Pia, katika (f) ambapo kuna sauti /ʃ/ badala ya /ʧ/.

e) Kuongeza maneno fulani ambayo ni lazima yatumike katika utamkaji wa lugha ya jamii fulani ambayo si lazima yatumike katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika (f) kuna utamkaji “hero rafiki” (Wamasai) ambapo neno “hero” limeingizwa katika tungo ya Kiswahili ikiwa si lazima liwepo.

Kihore na wenzake (1999) pia wamejadili dhana hii ya lafudhi na kutoa mifano ambayo haina tofauti na ile ya wanaisimu waliotajwa hapo juu kwa kuegemea zaidi upande wa vitamkwa tu. Wao wanasema kuwa lafudhi ni matamshi ya msemaji wa lugha fulani ambayo yanatokana na athari za kimazingira. Mazingira hayo wanayataja kuwa yanaweza kuwa ya kieneo, mahali alikosoma mtu na kiwango cha elimu. Wao wanatoa mifano ifuatayo:

*a)* *Nakwenda kurara* badala ya *nakwenda kulala;*

*b)* *Wamelipa mahali* badala ya *wamelipa mahari*;

*c)* *Wanachukia ushawi* badala ya *wanachukia uchawi*; na

*d)* *Walikunywa saidi* badala ya *walikunywa zaidi.*

Sanjari na wataalamu hao ni Habwe na Karanja (2004) ambao kwa hakika wameishia kuifasili tu lafudhi kuwa hutokea pale ambapo lugha inapombainisha mtu fulani na kumtenga kama msemaji au mwandishi mwenye mitindo ya kipekee ya kumbainisha. Wataalamu hawa hawakuendelea zaidi na dhana hii wala kutoa mifano. Aidha, wanazidi kuichanganya dhana hii ya lafudhi ambayo ni ya kimatamshi na mitindo ya uandishi.

## 4.0 Mtazamo wa Makala hii kuhusu Dhana ya Lafudhi

Katika makala hii tunabainisha kuwapo kwa aina mbili za lafudhi ambazo, badala ya kuziita lafudhi na lafudhi kali kama alivyoziita Massamba (2004), tunaziita lafudhi-nafsia na lafudhi-jamii. Lafudhi-jamii ni ile jumla ya utamkaji au uzungumzaji au usemaji unaowatofautisha wazungumzaji wa jamii fulani ambao unatokana na athari za lugha yao ya kwanza. Aidha, lafudhi-nafsia ni ile jumla ya utamkaji au uzungumzaji unaomtambulisha mtu fulani miongoni mwa wanajamii wenye lafudhi inayofanana. Tumeona ugumu kutumia "lafudhi kali" kwa sababu za kimantiki kwamba, mtu mwingine anaweza kusema kuwa tunaposema lafudhi kali tunamaanisha kiwango cha juu zaidi cha ujibainishaji katika utamkaji wa mtu fulani katika jamii yake au mtu anayetoka katika mazingira fulani. Hii inatokana na hoja kwamba kiwango cha kuathiriwa na lugha moja ya kwanza kinaweza kutofautiana kati ya msemaji mmoja na mwingine. Sambamba na hayo, tunaongeza kwamba, mbali na kuwapo kwa lafudhi-nafsia na lafudhi-jamii, lafudhi kwa ujumla tunaifasili kuwa ni utamkaji wa maneno ya lugha fulani ulio wa kawaida kama anavyoifasili pia Massamba (2004:44) katika kamusi yake ya isimu na falsafa ya lugha. Kwa mfano, lafudhi ya Kiswahili sanifu, Kibena, Kifipa, Kihaya, Kisukuma, na kadhalika iliyo ya kawaida kwa wasemaji wa lugha hiyo.

Hata hivyo, tumejaribu kuubaini msingi wa Massamba (2004) kuigawa lafudhi katika lafudhi na lafudhi kali kuwa ni wa kimatumizi na kijamii zaidi, hasa inapofikia hatua ya kuitumia dhana ya lafudhi kuonyesha utambulisho wa mtu binafsi miongoni mwa wenzake au mtu fulani wa jamii moja na jamii nyingine. Msingi huu ndio uliotufanya tuigawe dhana ya lafudhi katika aina hizo mbili zilizotajwa hapo juu. Tofauti iliyopo kati ya Massamba (2004) na makala hii kuhusu aina za lafudhi ni ya kiistilahi zaidi kama ilivyoelezwa hapo juu na pia yeye hakutoa ufafanuzi wa kina na mifano kuntu kuhusiana na lafudhi na aina zake. Vilevile, tunaona kwamba fasili ya dhana hii kwa wanaisimu wote tuliowagusia katika makala hii zinabeba chembechembe za kiisimu-jamii. Kwa mfano kuwapo neno "utambulisho" au yanayofanana na hayo kama vile "mazingira ya jamii fulani". Baada ya kujadili fasili na aina za lafudhi sasa tunaanza kuifafanua dhana ya lafudhi kwa ujumla na kisha aina moja moja kama ilivyoainishwa hapo juu na kutoa mifano.

## 4.1 Dhana ya Lafudhi kwa Ujumla

Katika makala hii tunaonyesha kwamba lafudhi haihusishi vipandesauti tu na vipengele vinavyohusu vipandesauti kama ambavyo imekuwa ikionyeshwa na wanaisimu wengi waliotangulia. Lafudhi imefasiliwa kuwa inahusu "jumla ya uzungumzaji" ambao unajumuisha vipandesauti, kiimbo, mkazo, toni, kidatu, wakaa na hata tambo. Kwa kusema hivi, tunapingana na Mgullu (1999) ambaye anavihusisha vipengele hivi katika kiimbo na kufasili kiimbo kuwa ni umbile la jumla la uzungumzaji wa mtu au kundi la watu fulani. Anaendelea kusema kuwa kiimbo kinajumuisha mambo yote yanayohusiana na uzungumzaji ambayo ni kidatu,

mkazo, toni, uzuri wa sauti na sifa nyingine zote. Kwa hakika, mwanaisimu huyu alikuwa anaelezea sifa za lafudhi ingawa yeye alishindwa kuelewa tofauti ya kiimbo na lafudhi. Hata hivyo, fasili yake, ambayo ninaiona kama fasili ya lafudhi badala ya kiimbo, inatoa picha kwamba kuna lafudhi ya mtu binafsi au kundi ambalo tumeliita 'jamii'. Kwa ajili ya welewa zaidi wa msomaji wetu, sina budi kutoa fasili za vipengele nilivyovihusisha na lafudhi kwa ufupi kulingana na wataalamu mbalimbali, ambazo pia tunakubaliana nazo kwani hatuna nia ya kuvijadili vipengele hivi kwa kina. Kugusia vipengele hivi kutatusaidia katika ufafanuzi wetu kuhusu dhana ya lafudhi.

> **Kitamkwa** kwa mujibu wa Massamba (2004:37-38) ni sauti dhahiri inayosikika wakati wa utamkaji maneno na ambayo inatambulika kialfabeti, kama vile: /p/, /t/, /s/, /a/, n.k.
>
> **Kiimbo** ni utaratibu maalumu wa upandaji na ushukaji wa mawimbi ya sauti zake (Massamba na wenzake, 2004:7).
>
> **Toni** ni sifa inayowakilisha kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi na ambayo huweza kubadilisha maana ya neno au sentensi hiyo kisemantiki au kisarufi (Massamba, *ktj*:87). Mgullu naye anasema toni ni kiwango cha kidatu pamoja na mabadiliko yake ambayo hutokea wakati mtu anapotamka silabi au maneno. Fasili hizi zote zinahusiana.
>
> **Mkazo**, Massamba na wenzake (*wtj*:8) wanasema kuwa ni kiwango cha nguvu inayotumika katika utamkaji wa silabi. Fasili nyingi zinakubaliana kuwa mkazo unahusu nguvu inayotumiwa katika utamkaji wa silabi fulani katika maneno.
>
> **Kidatu** ni sifa ya msikikosauti ambayo humwezesha msikilizaji kubadili kiwango chake cha sauti katika usemaji, kuanzia chini kwenda juu bila kujali kasimawimbi yake (Massamba, 2004:30).
>
> **Wakaa** ni jumla ya muda unaotumika katika kutamka sauti au silabi (Massamba, *ktj*:116).
>
> **Tambo** ni mwongezeko au mpunguo wa msukumo wa hewa ambao hutokana na mawimbi ya sauti kutoka hali ya mtuo na ama kupanda au kushuka (Massamba, *ktj*: 85). Kwa ufafanuzi zaidi tambo huhusu kasi ya msemaji katika utamkaji wake.

Kutoka katika fasili hizi tunaweza kuthibitisha kwamba lafudhi ni jumla ya utamkaji na uzungumzaji kwani kila kipengele ni lazima kihusishwe na utamkaji. Vipengele kadhaa miongoni mwa hivi vinaweza kutumika kwa pamoja katika lugha fulani na

vingine katika lugha fulani, huweza kutofautisha maana au kuwa na uamilifu fulani wa kisarufi.

Ama kuhusu lafudhi, si ajabu kusema kwamba jumla ya vipengele hivi ndivyo huitambulisha lafudhi ya mtu au kundi fulani. Hata hivyo, ni vizuri tukaeleza kwamba si lazima vipengele hivi vyote vipatikane katika lugha moja. Hii ndiyo maana kuna lugha zenye toni au mkazo na si vyote viwili kwa wakati mmoja, yaani katika utamkaji wa neno moja. Lakini pia kuna vipengele vingine ambavyo ni lazima tu vitajitokeza katika usemaji wa lugha yoyote iwayo isipokuwa suala la uamilifu wa vipengele hivyo tu ambao huweza kuwa tofauti baina ya lugha na lugha. Kwa mfano, vipandesauti vipo katika kila lugha kwa sababu ndivyo sauti yenyewe, tambo, kidato na kiimbo na hata wakaa. Kwa lugha zilizo nyingi, toni na mkazo huwa na sifa ya kusigana ambapo kimoja kikijitokeza katika neno kingine hakiwezi kutokea.

Kwa kuwa vipengele hivi vinahusu utamkaji, ni dhahiri kuwa inawezekana kabisa msemaji wa lugha fulani, kama lugha mama yake, anaweza kuwa ameathiriwa na toni iliyo kwenye lugha yake na hivyo anapotamka maneno ya lugha nyingine athari za toni za lugha yake huweza kujitokeza na hivyo kumtambulisha kuwa yeye ni wa wapi. Aidha, msemaji anaweza kuwa ameathiriwa na mkazo au wakaa ulio katika lugha yake, na hivyo anaweza kutamka maneno ya lugha nyingine kwa kuweka mkazo katika silabi inayofanana na ile ya lugha yake au kuweka wakaa mrefu au mfupi katika irabu ulio kinyume na lugha tofauti na lugha mama yake na hivyo, kumtambulisha kuwa yeye anatoka katika jamii-lugha fulani. Pia kwa msemaji fulani anayetamka maneno fulani ya lugha isiyo lugha mama yake anaweza kudondosha sauti fulani katika utamkaji wake au kuingiza sauti isiyokuwepo katika lugha hiyo anayoitamka kwa sababu tu ya athari za lugha mama yake. Vile vile, msemaji huyo anaweza kulazimisha kubadili kitamkwa fulani katika neno kwa kuwa kile kilichopo katika neno la lugha anayoisema hakipo katika lugha mama yake na hivyo akashindwa kuitamka sauti ile na kuchopeka sauti inayokaribiana na ile iliyopo. Kwa mfano, Mkurya kutamka **/r/** mahali pa **/l/** katika neno anapotamka maneno ya lugha ya Kiswahili kama vile "**kulala**" wao wanasema "**kurara**". Sauti /**r**/ ni kilainisho na kama ilivyo /**l**/ lakini /**l**/ haipo katika utamkaji wa lugha ya Kikurya.

Hata hivyo, ni vema ieleweke kuwa lafudhi-jamii na lahaja ni tofauti. Lahaja inahusisha vitu vingi zaidi ikiwa ni pamoja na msamiati, semantiki, na kadhalika ilihali lafudhi inahusu usemaji au utamkaji tu (Mkude, 1983).

### 4.1.1 Lafudhi-nafsia

Kama tulivyoifafanua hapo awali, hii ni lafudhi ya mtu mmoja mmoja inayoitambulisha nafsi yake katika jamii lugha moja na yenye lafudhi-jamii moja. Lafudhi-nafsia inatambulishwa na vipengele mbalimbali vya kimatamshi kama vile

uzito au wepesi wa sauti, ukali wa sauti (ambavyo Mgullu anaviita uzuri wa sauti), tambo, uvutaji wa sauti, ufinyaji wa maneno, kigugumizi, mkwaruzo wa sauti, usemeaji wa puani, kidatu cha juu, kati au chini, uongezaji wa sauti katika utamkaji wake usio na umuhimu na urefushaji wa sauti. Hii ni sawa na lahaja-nafsia ambayo ni usemaji wa lugha ambao huwa ni mtu binafsi (Massamba, 2004:44). Hata hivyo, lahaja-nafsia inaenda ndani zaidi ya lafudhi kwani inaweza ikahusisha hata vijineno au maneno au virai fulani kama alivyozoea mtu fulani kuyatumia katika usemaji wake tofauti na wengine. Kwa mfano, virai kama vile: ee bwana, jamani, unaona bwana, sawasawa?, na kadhalika. Lafudhi kwa upande wake inahusisha utamkaji tu na si maneno au virai.

Katika utamkaji wa maneno yale yale katika tungo fulani, wasemaji huweza kujibainisha nafsi zao kuwa huyu ni tofauti na yule hata kama msikilizaji akiwa nje na msemaji akiwa ndani au mahali popote asipoonekana. Kuna watu katika jamii-lugha zetu wana sauti nzito sana na ya chini au nyepesi kiasi au sana na ya juu (au kali) kimsikiko kiasi cha kuwabainisha pindi wanapozungumza katika usemaji wao wa kawaida. Aidha, wengine wanapoongea huwa wanatamka maneno haraka haraka sana, ambao aghalabu hufinya maneno na baadhi ya sauti. Kwa mfano, si ajabu kumsikia msemaji wa Kiswahili akisema "*sa(sa) mi(mi) n'tafanyaje*?". Silabi zilizofungiwa mabano mara nyingi hudondoshwa katika usemaji huo. Wengine huzitamka kabisa silabi zote lakini ni kwa haraka haraka sana.

Pia, kuna wale ambao wanatamka maneno kwa kuvuta sana sauti zao na kurefusha irabu kama vile, "*saaasa miiimi nitafanyaaaje*?" na aghalabu usemaji wao huwa wa taratibu taratibu. Wengine wana kigugumizi, yaani wanapata ugumu wa kutamka sauti katika maneno na hivyo kujikuta wanarudiarudia baadhi ya sauti. Baadhi yao huwa na kigugumizi kikali na wengine wastani. Kwa mfano, utakuta wanatamka; "*sa-sa-sa- sasa mi-mi-mi- mimi nitafa-nita-nitafanyaje*?" Wengine sauti zina mkwaruzo kana kwamba wameongea sana kiasi cha koo kukauka na wengine kusemea puani hata sauti ambazo si za puani kama vile; "sa`sa` mi`mi` ni`ta`fa`nya`je`?". Alama ya wimbi juu ya sauti inaashiria unazali. Baadhi ya wasemaji wa lugha fulani huwa wana tabia ya kuongeza sauti au vijineno fulani katika utamkaji wao au mighuno fulani na hivyo kujibainisha kibinafsi miongoni mwa wasemaji wengine wa lugha hiyo hiyo; kwa mfano, "*sasa, eh, mimi nitafanyaje* (*bwana*)?*, "aaa, sasa mimi nitafanyaje*?, n.k.

Kitu kingine ni kwamba, hata kama utawaweka pamoja watu wenye kigugumizi, kwa mfano, bado watajibainisha nafsi zao kwa utamkaji wao kwani katika kigugumizi huweza kuongezeka na uzito au wepesi wa sauti, urefushaji wa suati, na kadhalika.

### 4.1.2 Lafudhi-jamii

Lafudhi jamii inajumuisha vipengele vya matamshi ambavyo huweza kutofautiana baina ya jamii-lugha moja na nyingine. Vipengele muhimu ambavyo vinaweza kutumika katika kuibainisha lafudhi hii ni kama vile mkazo, toni, wakaa, muundo wa sarufi ya lugha na kuwapo au kutokuwapo kwa vitamkwa fulani katika lugha hiyo. Hujibainisha kwa ukali zaidi pale ambapo msemaji wa lugha yenye kipengele fulani kati ya hivyo, na chenye nguvu au uamilifu mkubwa katika lugha yao, atakuwa akisikilizwa na msemaji wa lugha nyingine yenye kipengele kingine au hichohicho lakini hutofautiana viwango vya ukali wake. Nadhani hapa ndipo Massamba (2004) alipopatia msingi wa kuigawa dhana ya lafudhi kama lafudhi na lafudhi kali.

Wataalamu wengine waliozungumzia dhana hii walikuwa wanazungumzia zaidi aina hii ya lafudhi ambayo hata hivyo, kwa mtazamo wa makala hii, walikuwa wanahusisha kipengele kimoja au viwili tu vinavyohusika katika lafudhi, yaani vitamkwa na sarufi tu.

Mifano:

(i) Utambulisho wa lafudhi kwa kigezo cha *vitamkwa*:

*Wafipa: Nguo hii ina samani kubwa (kitamkwa /s/ badala ya /ɵ/*

*Safali hii ni ndefu sana (kitamkwa /l/ badala ya /r/*

Hii ni kwa sababu katika lugha ya Kifipa sauti /ϴ/ na /s/ na sauti /l/ na /r/ si bainifu, zote hutumika kwa kubadilishana.

(ii) *Toni*

Wasemaji ambao lugha yao ya kwanza ina toni huwa wanaathiriwa na toni hizo na kujikuta kila maneno wanayotamka, haijalishi ni ya lugha gani, hufuata ruwaza ya toni hizo bila kujijua.

*Sasa mimi nifanyéjè*? [---- ] (alama (`) huonyesha toni chini na (´) toni juu

Katika utamkaji wao wa maneno ya Kiswahili utakuta wanaathiriwa na ruwaza ya toni za lugha yao na hatimaye kujibainisha kwamba wao ni watu wa jamii-lugha mama gani. Aidha, kiimbo katika utamkaji wao huwa kinapanda katika silabi ya mwisho kasoro moja na kushuka katika silabi ya mwisho. Utamkaji huo ndio unaojidhihirisha wanapotamka maneno ya lugha ya Kiswahili. Hali hii inajitokeza sana kwa wazawa wa lugha yenye toni wanapotamka maneno ya lugha ya Kiswahili.

(iii) *Mkazo*

Kwa wasemaji wa lugha ya kwanza ambayo ina mkazo huwa wanalazimika kutamka maneno ya lugha yoyote ile kwa kufuata ruwaza ya upachikaji mkazo ya lugha yao hiyo ya kwanza na hatimaye kujikuta wanajibainisha kuwa wao ni wasemaji wa lugha gani. Hili tunaliona kwa wasemaji wengi wa lugha ya Kiswahili wanapotaka

kuyatamka maneno ya lugha nyingine za Kibantu yenye toni. Wao hushindwa kuibaini toni vizuri kwa sababu huwa wanatamka kwa kuweka mkazo katika silabi ya mwisho kasoro moja. Hivyo, hujibainisha kwa haraka sana.

Kwa mfano: Neno la Kihaya "*okwihyúla*" – kupakua chakula, msemaji wa Kiswahili atalitamka "*okupaku'la*" (alama (') huonyesha mkazo badala ya kutumia tonijuu (´). Tofauti hizi kimatamshi ni kubwa sana kiasi cha kuweza kumbainisha msemaji kuwa ni wa jamii-lugha gani au lahaja gani.

Wasemaji wa Kiswahili sanifu walioathiriwa na matamshi ya lugha ya Kiarabu huwa wanaweka mkazo katika silabi ya kwanza au ya pili badala ya silabi ya mwisho kasoro moja kama ilivyo kawadia ya utamkaji wa maneno ya Kiswahili sanifu. Hii inaonyesha kwamba katika lugha ya Kiarabu maneno huwa na mkazo katika silabi ya kwanza au pili ya neno.

Kwa mfano: "*Fa'hamu*" badala ya "*faha'mu*"

*Mu'stafa* badala ya "*Musta'fa*"

*Kuba'riki* badala ya "*kubari'ki*"

(iv) *Wakaa*

Aidha, kuna wasemaji wengine wanaotambulishwa kwa lafudhi yao kuwa na uvutaji au urefushaji wa sauti.

Kwa mfano, Mbena akiuliza swali anaweza kusema:

"*Kwani huyu mtoto wa n:ani*?

"*Yeye ni mt:oto*?" (alama (:) huonyesha urefushaji wa irabu hizo.

Kwao wanapouliza swali hutumia urefushaji wa irabu, hasa kwa silabi ya mwisho kasoro moja na neno la mwisho na kiimbo hushushwa chini (kwa mujibu wa uzoefu wangu katika kuyasikiliza matamshi yao baada ya kukaa nao kwa muda mrefu kidogo).

Kwa upande wa athari za kisarufi, tunaweza kusema kuwa baadhi ya lugha, kama vile lahaja fulani za Kisukuma na Kinyamwezi, mofimu inayoonyesha hali timilifu au mazoea huweza kutumia kiambishi {–ga} mwishoni mwa neno.

Kwa mfano, Kinyamwezi:

"*Nakasanga waya**ga***" (Nikakuta amekwenda)

au "*Ene nuyombaga mihayo misoga du*" (mimi huwa ninaongea mambo mazuri tu).

Kutokana na kuathiriwa na kuwapo kwa kiambishi hiki katika maumbo ya maneno ya lugha mama kama hii, basi wasemaji wake huweza kujikuta wanatamka maneno

ya Kiswahili kwa kuongeza kiambishi hicho wakiwa na dhana ileile ya lugha mama. Mara nyingi wasemaji wa lugha kama hii wanapotamka maneno ya lugha ya Kiswahili utasikia wakisema:

*Huwa nakuta ameondokaga*

*Yeye anaondokaga mchana*

Pia, kushindwa kutamka sauti vizuri kama mzawa au kutofuata upatanifu sahihi wa kisarufi wa lugha inayosemwa huibanisha lafudhi ya mtu. Hata hivyo, kushindwa huko au kukosea huwa kunatokana sana na athari za lugha ya kwanza. Kwa kutumia misingi hii, unaweza kuelezea kwa nini lafudhi ya msemaji fulani inajibainisha anapotamka maneno ya lugha ya Kiswahili. Athari hizo, ambazo wataalamu wengi huziita za kimazingira, huwa zinatokana na vipengele hivi tulivyovitaja na kuvitolea mifano baadhi yake. Vipengele vinabainika zaidi unapowasikia wasemaji wa lugha fulani wanapojaribu kutamka maneno ya lugha nyingine isiyo lugha yao ya kwanza.

## 5.0 Hitimisho

Tunahitimisha kwa kusema kwamba, dhana ya lafudhi ni pana na inahusisha vipengele vingi vya kimatamshi zaidi ya vitamkwa. Vitamkwa na utamkaji wake ni sehemu ya lafudhi. Lafudhi ni dhana pana na inahusisha vipengele vyote vinavyosikika katika uzungumzaji wa lugha. Vipengele hivyo ndivyo vinavyombainisha ama mtu binafsi katika jamii-lugha yenye lafudhi-jamii moja au mtu wa lafudhi-jamii fulani anapoingia katika jamii yenye lafudhi-jamii tofauti. Aidha, ieleweke kuwa tunaporejelea lafudhi-jamii tunamaanisha lugha fulani na utamkaji wake. Kuna mwanya unaohitaji kufanyiwa utafiti katika eneo hili kwa kufanya utafiti linganishi ili kuzichanganua kwa kina na kiisimu sababu zinazowafanya wasemaji wa lugha mama fulani kujibainisha kwa jinsi hiyo wanavyojibainisha katika utamkaji wao wa maneno ya lugha ya Kiswahili tofauti na wasemaji wa lugha mama nyingine. Pia unaweza kufanyika utafiti katika jamii ya watu wa Dar es Salaam na tofauti zao katika matamshi ya Kiswahili sanifu kama mada ya uwanja wa isimu-jamii.

## Marejeleo

Ali, M. (1976). “Lafudhi ya Kiswahili” katika *Uandishi wa Tanzania: Kitabu cha Kwanza-Insha*, Nairobi: EALB. kur. 108-113.

Habwe, J na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Kihore, Y.M. na wenzake. (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Maganga, C. (1976). “Matatizo ya Lafudhi ya Kiswahili” katika *Uandishi wa Tanzania: Kitabu cha Kwanza-Insha*. Nairobi: EALB. kur. 88-91.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B na wenzake. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Mkude, D.J. (1983). "Mtawanyiko wa Lahaja za Kiswahili". Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I: Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 62-81.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.